Com.Ayonga: Mama ulikuwa umesema kwamba Kenya tuwe na vazi ambalo linaweza kutututambua kama wa Kenya, ukatoa mfano wa Uganda, ukatoa mfano wa Nigeria, lakini hukutuambia vazi hilo ni lipi? Kwa maana ni rahisi kusema lakini hukutusaidia kwa kikatiba kwamba unataka wa Kenya wavae namna hii au ile,.

Zainabu: Hapo mwenyekiti, ningependa vazi ambalo linaheshima kama ndege, round, ama nguo yoyote refu ambayo inaheshima katika nchi yetu.

Com.Nunow: Asante sana nafikiri itakuwa shida kutafuta ni nini Kenyans itawatambua, wewe umesema kwamba ungependa kuona Kenyans wakitambulika kwa mavazi yao, na nafikiri hiyo tumekuelewa kabisa. Ingekuwa Commissioner alikuwa anataka kama una idea tayari lakini inaonekana hujafikiria kwa hivyo inaweza kuwa jambo ambalo Tume itaangalia, tafadhali ujiandikishe pale. Mathayo Magova.

Matayo Magova: Kwa majina mimi naitwa Mathayo Magova, naonelea upande wa land, kwa sababu hii land imechukuwa pesa kutoka kwa shamba lako, na hii shamba wewe uliwachiwa na baba yako sasa watu wa land wanachukuwa pesa nyingi wanagawa wananunua shamba letu.

Ya pili, kesi ya land haingefanyiwa kortini, hiyo ingefanyiwa nyumbani kwa sababu korti haijui habari ya land, na kuna wazee wa karibu wanaojua habari za land huko nyumbani kwa nini wanapeleka hiyo kwa korti?

Ya tatu hapa sisi watu wa District ya Busia, kitu kilikuwa inatupa sisi nguvu za kulima ilikuwa pombe ya mulicha, wewe unatengeneza pombe ya mulicha na watu wanakuja kusema watu washikwe siku moja. Sasa hiyo yote njia ya mapato serikali imefunga na kuna watu wengine hawana nguvu, watapata chakula namna gani? Ni hayo tu.

Com.Nunow: Kwa hivyo umesema pombe ya kienyeji ihalalishwe, iwepo? Asante sana tafadhali ujiandikishe kwa hiyo register. John Makanga

John Makanga: Yangu ni machache, John Makanga kitu mimi nilikuwa naonelea, mambo ya wabunge ambao wamesimama kura kupeana pesa wakati wa kura, kutokea mwaka huu ambao kura inakuja, iwe sheria mtu yeyote akipatikana akipena pesa, kura yake hiyo waaribu wapewe yule ambaye anamfuata, kwa shauri imekuwa tunachagua wabunge wengine ambao hawawezi kusaidia kwa vile wako na pesa, mtu anakaa Nairobi miaka kumi atakuja kupeana pesa.

Jambo la pili, kura hizi ambazo zinakuja mbele, President asichague mtu raia sisi wenyewe tuchague hapa mtu, wenyewe wasimame huko Nairobi halafu tuanzie hapa kupiga kura kama ni watu watano wasimame wote watu watano sisi tupige kura kutoka hapa, yule mwenye atapatikana ameshinda ndio akuwe President sio mtu mmoja ku appoint President.

Jambo la tatu, mahakama kuu, ichaguliwe na Bunge. Wabunge wa High Court, wa bunge ndio wachague ma-judge, sio mtu mmoja kuchagua halafu ndio anajuana na huyo mtu, atakuwa ana m-safe wakati yuko na makosa. Ma-judge ambao wanafanya kwa High Court wachaguliwe na wa-bunge na Bunge wapige kura kupendekeza wale majudge ambao wanafaa. Kile kitu naongeze kabisa, mbunge yeyote ambaye atapatikana anapeana pesa, ndio apite hiyo kura iharibiwe, wapee yule ambaye anamfuata kwa shauri hiki kitu kinafanya tusiweze kupata wabunge waziri, yangu ni hayo tu.

Com.Nunow: Asante sana, inaonekana chairman anasumbuliwa na hii corruption ya elections kwa hivyo ana haki ya kusema nini inamsubuwa na maoni yake. Mzee Andrea Mzungu huyo mzee aje mbele, tafadhali muandikishe.

Andrea Mzungu: Jambo wakubwa wote, nimefurahi sana kwa kuja hapa, ili nihudhurie mkutano huu, sisi ni watu vilema ambao tuliwakilisha location ya Bohaya. 1948, wakati chief Ezekiah alipokuwako, tuliishi Nairobi miaka nane tukisomea shule ya Institute for the blind, wakati huo Principle wetu alikuwa Hezbone, ndio Hezbone huyo ndiye alitufunza masomo. Na tulifurahi kwa Lucy Braille ambaye alianzisha masomo ya Braille. Tena na ule Miss Valo Nekonovallo, hao ndio walikuwa nuru yetu wasio ona, na leo President wetu alichukuwa, a jukumu kuwa mdhamini wetu, kwa sababu wakati wa emergency tuliambiwa ya kwamba vilema wote wale wako katika Institute for the blind muunge mkono uhuru kwa sababu mtapata matunda. Na kweli pocket money ile tulikuwa tukipata tuliwapa, wakati bwana Peter Koinange mtoto wa Mbio Koinange alipoenda uingereza walichanga pese nyingi, na sisi vilema tuliunga mkono. Wak

Ya pili alichukua Josephine Sinyo kuwa mtangulizi katika blind school kuwa mjumbe maalum, tulipongeza na kitu kibaya, ambacho sisi tunaona hasa watu wa District ya Busia, President and million 72, President aliacha kutoa pesa bwana Mahewa alitangulia kutoa milioni kumi na nane hadi akifika milioni kumi na nne. Sisi hatupokei hata msaada hata wengine manyumba yanavujwa na hatuna mtu wa kutuangualia, wengine tuna watoto walikosa kuenda shule kwa sababu sisi hatuoni na hutana mapato, hatuna kitu chochote, Je nauliza wakubwa wa Busia hamuwezi kusaidia wasiojiweza? Mtasaidia nani mkikosa kutusaidia sisi? Kutokea ma-chief ma-DC ma-DO, ndio macho, chief ndio macho ya DC na sub-chief ndio macho ya chief, basi kwa ufupi ningependa mchango huo bwana Mahewa akitoa wachague wajumbe wanao husiana group hiyo. Watembelee vilema wale walionadikwa katika government ili tuwe tupate kidogo tuwachie watoto wetu. Mimi nilisomea pesa ya ANC na

nilijifunza agriculture British Royal Commonwealth Blind society ilitoa pesa ya kujaribu kwenye afrika walitoka Kenya. Tulijifunza tukafaulu mimi nilikuwa grade two ya Agriculture katika blind school, sasa hiyo yote imezimia watoto wangu wanasema ulienda kusoma maharagwe ama ulienda kusoma mikate. Tafadhali President kama ungali wewe ndio mdhamini wetu, tuma wajumbe wache watuungalie tabu zetu kufuatana na watawala wako chini. Tafadhali Katiba ya sasa, ihalarishe wezi wakiingia boma ya watu na wakisikia yowe, wananchi waikimbilie usalama kuokoa wengine.

Kisa kingine kilitendeka huko Sidende kwetu wezi wanachokesha watu na kuwanyang'anya ng'ombe lakini kitu cha ajabu walienda kwa boma ingine kunyang'anyana ng'ombe vijana walipoondoka kuenda kuweka kizuio kwenye barabara, wezi walipiga simu kuambia police ati majambazi wako Sidende, neno la aibu walikuja police kubembereza vijana wakawachukua pamoja na maguru wenyewe wakapalekwa cell, kutoka hapo chief asubuhi yake hakufuata kusema ukweli mbele ya police hati hapana, hawa watu si majambazi walikuwa wanaokoa hata sasa kesi iko huko, je tutajua Toroitich Daniel Arap Moi anatawala nusu Nairobi, na nusu Kenya na Busia hapana, tunatawaliwa Uganda, ama Kenya? tafadhali tunaomba tusiwe adui wa police tusiwe adui wa chief, police wasiwe adui wetu mbali tuwe raia tuchanganyike, police wasikie mawaidha ya raia, na raia wote wasikie mawaidha ya police. Na kitu ambacho ninaona ikiwa mnasema ni uongo sisi tuli-feel form ingine hapa niko nayo, sisi hatukupata hata tangu sikupata hata msaada wowote. Yangu ni hayo tu.

Com.Kangu: Mzee Anderea, umesema mambo mengi unasema michango ya pesa imetolewa hamkupata kitu? Tungependelea utuambie tungependa walemavu wafanyiwe hivi, wafanyiwe hivi, umesema wewe umesoma na watoto wanauliza ulisoma nini? pengine mimi nafikiria ulikuwa unataka kusema kama walemavu wamesoma wasaidiwe wapatiwe kazi, nao wawe wanaweza kuwa na mapato. Ungekuwa unatuambia hivi ndio tungependelea ingetusaidia sana.

Andrea: Sasa wale walemavu wenzangu wapatiwe kazi, na mimi wanisaidie ikiwa pesa iko wanijengee nyumba kidogo ama wanipe ya kufanyia kazi yangu ya shamba kwa maana mimi pamoja na bibi yangu sasa tumekuwa wazee na watoto wangu hawana elimu hawana mapato, ndio hayo tu.

Com.Nunow: Asante sana mzee kwa hayo maoni, Christopher Wabwire,

Christopher Wabwire: Mimi kwa majina naitwa Christopher Wabwire, Maoni yangu nitasema pengine tulipata uhuru nusu kwanini niseme nilipata uhuru nusu? pia tulipata democracy nusu. Kama kila kitu tulipata huru, matembezi peke yake uwe ukitembea njiani ati unatisha sisi kutembea kwa sababu ya kutembea na chupa kama hiyo, wakiona umebeba ya taa watafikiria wewe unabemba chang'aa na sisi wazee tunashangaa hatujui kama chang'aa kuna bunduki ndani inatoka kuenda kuawa watu. Hiyo kama sisi tunasema ya kwamba tulipata uhuru na kila siku tunaimba hata kuwa kiongozi wa nchi anasema asiyezingatia utamaduni wake yeye ni mtumwa. Na je sisi kama utumwa zamani kulikuweco kitu kinaitwa kwa Kihayo ishushu ile mahali ya kukaa kutengeneza maneno kama mtoto wa fulani ni mbaya au fulani ni mzee mbaya wanakaa, wanazungumzia, ilikuwa pombe ya mlija, pia wakati wa kulima tulitumia pombe ya mlija na tunasema na tununue pombe ya kizungu, sisi watumwa hiyo ndio

sababu ya kusema sisi tungali watumwa, au tulipata uhuru, na kama tulipata uhuru kwa nini tunataka kubadilishwa katika kitamaduni chetu?

Pili, mimi ninasema namna hii, watu hawa watu wetu wa serikali tulisema watoto wetu ni hawa police, hata Administration police, hata assistant chief, hata na chief, police, wametuweka sisi kua adui, sisi wazee hata tukiona police tunataka kujificha. Kwa sababu siku hizi police ukizungumza kidogo akisikia wewe anaweza kukushika na kukupeleka huyo anakuwekea bangi na hiyo bangi ambayo wanashika watu nayo njiani wanaweka katika ma-ofisi yao, kwa nini? kama tulipata uhuru kweli kabisa. Mtu anaweza kufa hapa, pengine apigwe na jambo fulani, na chang'aa iko kwa njia huko wanawacha mtu hapa anakufa, wanakimbilia mtu wa changa'aa sasa watakuwa wamemsaidia huyu? Kushika mtu wa chang'aa, Jambo la pili, sisi kama tulipata uhuru na uhuru unasema demokrasia ni uchaguzi, kwa nini tufanyie likuru uchaguzi? Kwa nini hatufanyii assistant chief uchaguzi na chief? Kwa sababu niliyo sema hivyo mtu hawezi kuwatawala yule ambaye hawampedi sababu sisi zile zinatolewa tu, na anatulazimisha nikisema leo iko katika amri, iko amri kumi ya Mungu na iko sheria, sasa sisi tuko kwa sheria hatuko kwa kufuatilia mamb ya utamaduni wa haki wa kutawala uhuru wetu, kwa sababu.....

Interjection Com. Nunow: Mzee Wabwire, tafadhali utuambie mapendekezo, unasema chiefs, na sub-chiefs wachaguliwe sema hivyo usiulize maswali. Kusema ningependa namna hii, namna hii,

Christopher: Ningependa assistant chief achaguliwe, la pili assistant chief akisha chaguliwa, afanyiwe transfer kama DO, DC, na viongozi wengine. Pendekezo lingine kwa sababu, sioni kazi ya assistant chief anayofanya sasa kwa nini hawezi kudhibitisha na kuidhinisha huyu liguru achukue nafasi ya assistant chief kwa sababu kila wakati liguru ndio hufanya kazi katika area,

Interjection Com Ayonga: kwa hivyo unataka assistant chief atolewe? Au unapendekeza aje?

Christopher: Ninapendekeza liguru aidhinishwe afanye ya assistant chief, assistant chief atolewe.

Interjection Com Nunow: Can we have silence we will not proceed until you are dead silent.

Com.Kangu: Tulisema mwanzo mtu anazungmza hapa, tunanasa kwa mpango ya kunasa sauti, na mkipiga kelele, mtambo unanasa kelele wakati tutakaa chini kuanza kusikiliza wale hawakuwa (luhya dialect.....)

Christopher: kwa ingine tena wale watumishi wa serikali kama Police, AP, pendekezo langu ningesema hawangemaliza miezi sita, wakifikisha miezi sita wnapewa transfer kwa sababu hawajajulikana na watu, na hiyo ndio hufanya wakashajuana wanakuwa ma- adui, hiyo itatusaidia sisi.

Katika upande wa elimu, sisi kuna watu wengine ambao hawajiwezi, na tuliambiwa juzi, juzi ya kwamba hakuna fees katika

Primary schools, na saa hii hulipwa pesa zaidi kuliko hapo mbeleni ningependekeza hivi, ikiwa imepitishwa ya kwamba watoto hawalipi kitu, hata building fund vile vile watoe kwa kila kitu, Kila kitu ndani ya shule, watoto wasome kama zamani walipo anza.

Upande wa kazi, tumesema tunataka tuelimishe watoto kweli elimu tunataka tuwe na akili je pendekez wale watoto ambao wamemaliza training za teaching katika ualimu wamekaa nyumbani na tunataka tuongezwe wengine kwa vile pendekezo langu wangepatia first of all ambao walimaliza shule kwa training zao, wapate kazi ndio tuwapeleke wengine kwa shule tena pili,, nimi katika pendekezo katika watu wa Busia, tulihaidiwa ya kwamba tutapata TTC ningependekeza sisi katika Busia nzima mpaka Teso District hatuna training center yetu ya waalimu, tunaomba watuletee training college waalimu yangu ni hayo tu.

Com.Nunow: Asante sana mzee tafadhali ujadishe pale, kwamba umetoa maoni, Andrew Amahoya, Felix Muryani, Gerald Nyongesa. Reverend may be you could just make the announcement that you Rev. so and so is presenting the memorandum on behalf of Felix Muryani:

Wilson Ndindi: Majina ni Wilson Ndindi Magero Padre, Felix Muryani ni babu yangu nyinyi mnajua inaonekana kwa sababu ya uzee ameenda kutafuta lunch na amejiandikisha, ameniachia nimshikie memorandum yake. Kwa hivyo ninapeana memorandum yake kama written memorandum asanteni sana.

Gerald Nyongesa: My names are Nyongesa Gerald Muchui. I come from Khama Location. My views are:

Education: Education should be free to all Kenyans from class one to eight, because most of our pupils drop out in those levels. High levels should be shouldered by parents. In that regard a parent may be preparing for the eight to b selling something to ensure that his child or her child prospers in education.

Secondly, employment: let there be no quarter system, in that tribalism has always been portrayed because many people have undergone courses but because they have no persons in charge they will always lose their chances to get for somebody who has not qualified because of his or her father is in position.

Thirdly, Local government. I believe our councilors should be form four leavers in that to ensure that he is adequate with the language in the council to know that he can also get something for his own area other than going there to sleep.

Fourthly, Executive: The President should not have all the powers of appointing his people in power and lastly, on Job; let there be one man for one job. Lets not have this idea of people grabbing offices when others are just outside walking, tarmacking as if they have never qualified for such offices. Last these retirees who have at least enjoyed the economy of our country should leave to those people who are still young in the field to also enjoy the fruits of Kenyans, other than is somebody

for example comes an election where by old retirees are the people to work in offices while our form four leavers are growing poor and poor in our homes. Those are my views thank you.

Com.Nunow: Thank you very much Gerald for your views, please sign the register for us, Chrispinus Makhoha.

Chrispinus Makhoha: Memorandum yangu siyo ya kuandika ni ya kuongea,

Number moja, majina naitwa Chrispinus Makhoha vile mumesikia nikiitwa, memorandum yangu sio ya kuandikwa ni ya maneno, naongea kidogo,

1. Muundo wa serikali, katika miundo ya serikali ningependelea serikali ya majimbo sio serikali ya ofisi kuu. Na ikiwa itakuwa serikali ya ofisi kuu, ikiwa itakubalika Rais awe huko juu, na tuwe na majimbo hapa chini singependelea serikali ya uf alme. Ya kusema mtoto wa fulani akitoka ni mtoto wa fulani anaingia hapana, kwa hiyo serikali ya majimbo ningependa wananchi wachaguwe kutoka kwa governor mpaka kwa liguruu, na huyo liguruu alipwe mshahara.
2. Nimejaribu ninafikiria nimeguzia hiyo kuna wakati wanyama wa polini wanaharibu chakula cha watu, wakati mwingine wanaua hata mtu, serikali ya sasa, inachukua mnyama wa pori kuwa mtu wa maana sana kuwa kitu cha maana sana kuliko binadamu wa kawaida, mtu akiua mnyama wa pori nafungwa na mnyama wa pori akiua mtu, mnyama hafungwi, na tena wanamtetea, kwa hivyo ningependa hayo maneno yaangaliwe sana. Na mnyama wa pori akiharibu chakula cha mtu kwa sababu hiyo shamba ulipanda ndio ulikuwa unategemea, na hiyo pesa ulikuwa nayo wakati ule wa kupanda ilikuwa hiy, hiyo tu na utaona baada ya mnyama wa pori kuharibu chakula chako, unakaa miaka tano ndio ulipwe ridhaa, hiyo ni kunyanyasa mwananchi wa kawaida, unajua mimi ni kilema na ikiwa mnyama amebaribu chakula changu kilema, pesa ile saa ingine niliwaomba, kesho nitakula wapi? Nikiomba mnasema vilema wanaomba, omba, kwa hivyo ningependa, mnyama akiharibu chakula changu, wafanyiwe uchanguzi, kilikuwa kinatoshana namna gani mahali paliharibiwa na nilipwe papo hapo, na nilipwe kutoka katika District, sio kutafuta maneno ya kuenda Nairobi.
3. Mtu yeyote ambaye alikuwa akifanya kazi ya serikali aki retire tunajua serikali hupeana barua ya retirement kwa mda wa miezi sita hata wengine wanapewa mwaka mmoja, waalimu wanapewa hata zaidi ya miaka miwili, ikiwa umepewa barua ya ku-retire kwa miaka miwili, ningependa serikali iwe nayo inafanya juu chini huko juu, kujua Makokha ata retire kesho, ata retire baada ya miezi sita watengeneze benefit zangu, zitumwe siku ile mimi naenda nyumbani, niende na hizo zote, na nisirudi kuuliza, uliza.

Pesa za NSSF: Pesa za NSSF ziletwe katika District mahali ambapo mtu alikuwa anafanya kazi, saa ile ana retire, barua ya retirement ikija kwangu, ingine iende kwa hiyo ofisi kusema Makokha ata-retire kesho mmtengenezee marupu rupe yake ya retirement, ili nikitoka huko niende nichukue badala ya mimi kutoka huko na kuambiwa enda Nairobi, enda Nairobi, enda Nairobi. Ile pesa ilikuwa 10,000 saa ile nitapewa 10,000 faida yangu itakuwa 2,000 sasa hapo naona Katiba ya leo kama haisaidii watu, ni hayo tu asante kwa kunisikiliza.

Com.Nunow: Asante sana bwana Makhoha, kwa maoni yako, tafadhali ujadikishe Andrew Namange?

Andrew Namange: Nisie Andrew Namenge Kutoka Nambale township village Mariva. Maoni kange sava Katiba khale khwabechanga nesirero amera kanga niko Andrew Namenge khurula Nambale

Translator: I am called Andrew Namenge, from Nambale township Maliva village.

Andrew: Khale

Translator: Long time a go,

Andrew: Khwabechanga nende bakhulundu

Translator: We had elders,

Andrew: Muchinyanga sia siserero

Translator: during marriage times

Andrew: Tsinyanga tsa kifo

Translator: during death,

Andrew: Nende tsinyanga tsa arusi

Translator: and during weddings.

Andrew: Kwabechanga nende malwa ako bule

Translator: we had local brews from Wimbi.

Andrew: Isaino

Translator: These days,

Andrew: Ni khule nende bakini

Translator: if we have visitors:

Andrew: Kabila ngabo

Translator: like this ones

Andrew: Khunyola abasikari oli ngo welingialingia sa mungo ngoli mukini muburuchi

Translator: we find the askari's coming around and you look hopeless in the home in the midst of Administration.

Andrew: Savanga Katiba

Translator: I am pleading with the Constitution,

Andrew: Irulekhule

Translator: To release us

Andrew: Khube nende

Translator: so that we can have

Andrew: Ebindu ngebio

Translator: things like those

Andrew: kabendulakha

Translator: That are traditional.

Andrew: Eliakhubiri efew

Translator: Secondly,

Andrew: Efe badidi ba inyuma eno

Translator: We small citizens

Andrew: Sikhunyala khukula whisky

Translator: We cannot,

Andrew: Khubakeni abo

Translator: We cannot buy commercial beers like whisky

Translator: to our visitors

Andrew: Khuli nende

Translator: we have

Andrew: Abadekhi ba kando kando badidi

Translator: we have local brews in our homes

Andrew: Khusabanga Katiba

Translator: We are requesting the Constitution

Andrew: Ikonyekho ingira yosi yosi nga kha-factory

Translator: to look for ways and means where this can be made by a factory

Andrew: Abadekhi badidi badidi bano

Translator: These local brewers,

Andrew: Bairenge mu-factory omwo

Translator: should be taking these brews to that factory

Andrew: Okhulingara sawasawa

Translator: to analyse critically

Andrew: Malwa keni kakusibwengwe khumaduka au mu bar

Translator: so that these local brews are free from danger and they should be sold commercially in our public places.

Andrew: Khwefe abundu badidi

Translator: We the common mwananchi

Andrew: Khunyala khukulakho

Translator: we can buy

Andrew: Khulondana na mapato kefu ni kali madidi

Translator: depending on our meager incomes.

Andrew: Eliakhudaru

Translator: Thirdly,

Andrew: Abasikari nibola mungo

Translator: when the askaris reach our homes

Andrew: Bacha mpaka khubulire

Translator: they entreat our privacy

Andrew: mbara nibiakhuba mbu omundu mukhulundu khwakisa malwa khubuliri

Translator: seriously speaking, we as elders can we hide beer in our bedrooms?

Andrew: Abasikari abo babechanga sa nibenya abakhasi bali munyumba omwo.

Translator: Those askaris interest is not beer but they look for our wives.

Andrew: Nende ebindu bili khusitanda okhwo

Translator: together with our bedding.

Andrew: Ako niko kambere nako1

Translator: that is all I have.

Com.Nunow: Asante sana mzee Namenge kwa haya maoni tumeyapokea, utajiadikisha pale, na u-sign register asante sana. Kenneth Kafua, na baada ya Kenneth wajitayarisha wanafunzi wa Igara Secondary school.

Kenneth Kafua: Basi kwa majina ninaitwa Kenneth Kafua nitatoa maoni yangu. Nitasoma vile nilivyo andika, wananchi wa Kenya

Interjection Com.Nunow: Kenneth, usisome kama una maandishi utatuangazia, utakuwa unafanya kazi mara mbili sisi wenyewe tutasoma tupatie points peke yake.

Kenneth: Sawa ninapendekeza ya kwamba wananchi wa Kenya wakubaliwe kutoa maoni kulingana na Katiba ambayo inawatawala. Jambo lingine lugha ambayo itaandikwa katika Katiba lazima iwe lugha mbili ambayo ni ya kiswahili, na kiingereza ambayo inaeleweka. Katiba vitabu vitolewe ambavyo vinachapishwa na kila mwananchi apate kujua Katiba yake. Rais achaguliwe na wananchi wenyewe, Rais apewe utawala miaka kumi sio zaidi ya hapo, akiwa mzuri akiwa mbaya, miaka kumi tosha. Rais awe mtu ambaye amesoma vizuri na awe mtu ambaye anajua lugha mbili. Rais anyanganywe mamlaka kama ya detention, asiwe na mamlaka ya kufunga mtu, detention lazima ahukumiwe kortini, na huyu mtu atangazwe katika gazetti rasmi la serikali na apewe siku kumi nne kufanya appeal. Pia sheria ambayo inamuhukumu iandikwe katika gazetti rasmi ya serikali. Rais asiwe na mamlaka ya kunyang'anya wananchi kutembea katika nchi yao. Pia, Rais asikubaliwe kufuta mtu bila kupitia kwa Bunge.

Ningependa pia liguruu aangaliwe kama mtawala apewe mshahara, ili kusudi asiwe mtu wa kuomba ama kuleta ufisadi. Jambo

lingine ambayo ningependa kuguzia, TKK toa kitu kidogo, yule mtu ambaye anapeana hongo, na yule ambaye anachukua hongo lazima washtakiwe. Mwizi ama wizi, mtu yeyote ambaye aliiba mali ya umma na anataka kusimama Ubunge au Rais lazima ahukumiwe kortini na arudishe hiyo mali.

Ningetaka kuguzia mambo ya mipaka. Mpaka ambao uliwekwa na serikali ya ukoloni lazima uheshimiwe na usiodolewe kulingana na kitabu cha methali 22: 28 usiondoe alama ya mpaka wa zamani uliowekwa na babu zako.

Pia ningependa kuguzia mambo ya watoto. Mtoto lazima apewe elimu ya bure ikiwa ni msichana na ikiwa ni mvulana. Uridhi, nikizungumzia mambo ya uridhi, mzazi akiwa na watoto wawili ni sharti wapate uridhi kutoka kwa wazazi wao.

Mapenzi: Yule mtu yeyote ambay atapatikana akifanya mapenzi na mtoto ambaye ni wa chini ya miaka 18, sheria ichukuliwe andikwe na ahukumiwe bila kusitasita.

Ningependa kuzungumzia mambo ya ugonjwa wa ukimwi ambao umekuja, nauliza ya kwamba iandikwe kwa Katiba ya kwamba mtu akiwa na visuzi vya ugonjwa wa ukimwi, na anajua ya kwamba ana viruzi na anaendelea kusambaza, huyo mtu anastahili kushtakiwa.

Mavazi: Kulingana na tamaduni za mwaafrika lazima mavazi yaheshimiwe, mwanamke hastahili kuvaa mavazi ya mwanamume na mwanamume hastahili kuvaa mavazi ya mwanamke.

Kuo: Ndoa kijana na msichana, sharti achague yule kijana ambaye anataka kuo, ama kuoleka. Pia ninaguzia upande wa mahari. Lazima kuheshimu tamaduni za wafrika au mtu wa Kenya. Kitu kidogo kitolewe ili kuidhinisha ya kwamba huyu nimemchukua kama mke na heshima ikuweko kati ya haowatu wawili.

Disability: Ningependa kuguzia watu ambao ni walemavu: Walemavu lazima wasaidiwe sheria iandikwe, mlemavu yeyote ama kipofu serikali isaidie kimapato, kielimu na mambo mengine kadhalika.

Abortion: Nikuguzia mambo ya abortion kutoa mimba yule mtu ambaye atatoa mimba ambayo si halali ni sharti ashtakiwe.

Interjection Com.Ayonga: Halali ni nini?

Kenneth: Mimba ambayo haina baba ama mama. Basi ninamaanisha hivi, abortion mwanamke akipatikana akitoa mimba anafaa ashitakiwe.

Employment: One man one job, mtu yeyote ambaye ameajiriwa katika serikali yetu ya Kenya na ame-retire asikubaliwe tena

kurudi kwa kazi. Mtu anayetaka kazi ya ubunge lazima ajue kusoma, kuandika, asiwe mtu ambaye ako na record mbaya ya ufiada au muuaji. Mwenye kupenda maendeleo na kupenda nchi yake. Kila mwananchi wa Kenya anakubaliwa kupiga kura.

Lugha mbili ambazo ni kiswahili na kiingereza zikubaliwe kuongea katika Bunge. Vyama vingi vikubaliwe katika nchi ya Kenya.

Interjection Com Nunow: Endelea make your last point, one last point.

Kenneth: Point yangu ya mwisho angalau nimeandika mengi, kuanzia kwa utawala, Liguruu, sub-chief, na assistant chief wachaguliwe na wananchi. Asante.

Com.Nunow: Asante sana Kenneth usione hujamaliza kwa sababu tutasoma yote na itaingia kwa computer ya Tume. Wanafunzi mko tayari, Patrick Umachi, karibia pia Caroline Kelasi.

Patrick Omachi: I am called Omachi Patrick from Igara Secondary School, form four. I have some views. My first views goes to President and the power, I want the President's power to be reduced because he has a lot of power than other people. Also the power of the President should be shared by the Prime Minister and the Vice President. If the President has done something wrong either he has stolen the public money or other resources and his management is not good, should be forced by the Constitution to resign and then taken into the court and judged and if he has stolen public money he should be forced to repay that money or that property that he has taken from the government. Also the MPs whom we are electing, I want when you want to become the Member of Parliament should be retained and if you are the Member of Parliament and then you are not doing your work very well as an MP you should be forced by the Constitution or the people that you are representing in Parliament to resign, as we have had that, there are some MPs who went to the Parliament for four years, and then they have not said anything about their Constitution, those people should not be allowed to go back again to the Parliament.

In the public according to the public money and resources, that should be shared that every Kenyan should get that money to be shared equally because, there is some public money that has been used to build some places like the Province where the President or those who are in power have been used and some of us here, in Busia and in Teso District you get some roads, they are very bad, they are unaccessible to various places. So I want the Constitution to provide that the government should construct every road in the country they should be in good condition.

Also the Commission of enquiry should be set up because there are some things that have happened in this country whereby some people have been assassinated and some activities have come up due to reluctance on the part of the security force. The Commission is to be set by the Constitution to provide that the enquiry Commission should be set and if anything comes out in the country they can inspect anything and then that to be announced in public, because there are some activities that in 1992

whereby some clashes arose up and then a Commission was up and it has never given out its report.

In the area of education, we want Primary education to be compulsory and free education. Every Kenyan citizen or every Kenyan child should have a right to get education and should not be denied that right because the parents do not have anything. Also if a student in form two or form three has not received that certificate that shows that he has gone to school, the assessment test should be done and then to be given a certificate and some opportunities should be set aside for them because there are some people who have no certificate and are just staying at home and have at least gone upto form three.

Girls inheritance rights from their parents, I do not agree with that because, this will cause some chaos in the family. If a girl is married and inherits from the parents, she will not respect the husband. If a man

Interjection Com.Kangu: Kuna wale wameanza tena kelele, na tumesema huu ni mladi wa Kenya wote, boys equal, girls equal tumpe kila mtu nafasi yake ya kuzungumza.

Patrick: I want also to say that girls should get married at about 21 years, and anybody who is found marrying a girl less than 21 years should be prosecuted by the law and the man should marry when he is already 25 years and above. That means that when they marry at that age, they are capable and are mature enough to manage their family.

According to the office there are some people who are owning several offices. You get somebody who is a Permanent Secretary, and then he is also a Director in a certain Parastatal body. So I want if you are a Permanent Secretary, you just have one office just remain in that office and the other one whereby somebody is the secretary of the Cabinet and he is also the Chairman of the Civil Service, that one should be divided to create jobs for several other people.

Interjection Com.Ayonga: Omachi you have made your point one man one job, as simple as that without any explanation we know all those things, we are not foreigners, okay go ahead.

Patrick: If you are a civil servant I want to say this, you should be allowed to retire at the age of 60 years. If you retire, at the age of 60 years, as soon as you leave the job you are paid about 3 months before the retirement. Thank you.

Com.Nunow: Omachi asante sana, please sign the register, I now call Caroline Kerasi

Caroline Kerasi: Guests of honours and the rest before you is Kerasi Caroline from St. Pauls Igara. I have few remarks to pass across. One point to start with, the first is inheritance of properties by the girls. Girls should not be denied the right for land, reason is because a girl who is learned and knows the management of land, can start some projects that can assist the family.

Secondly is the early marriages to girls. Early marriages to girls should be abolished. This is because some parents insist their daughters to get married before 18 years. For the parents to get dowry.

Thirdly the Constitution should provide, that people should marry girls who are below 18 years should be arrested and be disciplined. Then lastly girls should also be given a chance to attain higher level of education. For me to say this is because boys are given chances for higher education because they are the people to remain and assist them, they forget girls if they are educated to higher levels they will assist the parents and they will participate in projects that will assist the fellow brothers and the entire village. Thank you.

Com.Nunow: Thank you very much Caroline, please let us have your paper, and sign the register and Hon.Phillip Masinde:

Hon Phillip Masinde: Hon. Guests dear Commissioners, you are welcomed to Nambale Constituency. I submitted my memorandum but it was a summary so what I have to say is not a summary of what I submitted but what I submitted is the summary of what I have to say and I hope you will patient with me, on whatever I have to say but I will try as much as possible to keep within the time limit.

Commissioners, Kenya Constitution I have a copy here of the current Kenyan Constitution, I have been looking at it for the past 10 years, I have also helped in mutilating some of the chapters and sections of the same. I want to say this, that God gave to Moses 10 commandments. Kenyan Constitution which is not within those 10 commandments that God gave to us is not the Constitution for Kenyans, because anything that is outside the Constitution which, or outside the Constitution which should be in the context of the 10 commandments is not for human beings. I want to take this opportunity to thank our fore fathers who had the opportunity to go to Lancaster House and negotiate the Constitution, that brought us Uhuru. That Constitution as far as I am concerned, was very relevant and many of its parts are still relevant. It was however destroyed by the Kenyans who were a bit too hungry for the power, or who were selfish, and they created sycophan who mutilated the Constitution to what we have now.

At independence our former freedom fighters aimed three very important things for the Kenyans.

1. To eliminate ignorance,
2. To eliminate sickness
3. To eliminate poverty.

It worked for a short time unfortunately, because of the mutilation of the Lancaster Constitution, all that they vowed to eliminate has back in a bigger way, than they found. We find that recently our MPs passed that all children should go to school compulsory. Unfortunately we do not have enough teachers, we do not have enough facilities to get all the school going children to go to school, and we are making a law which we know is going to be broken not because of the wish of anybody,

but because we have failed to prepare so as to make that law to be followed.

The next thing we have problems the children that are able to go to school at the moment are lacking facilities, they have no books, they have introduced so many things in Primary schools, so many funds which are unchecked and uncontrolled, that are affecting education of all Kenyans. We have primary school children they are sent away from school after every other day, to collect 20 Kshs. for a watchman, 5 Kshs for water I do not know 20 Kshs for the teachers breakfast or lunch, I am ex-teacher, all these people are working in the offices, the people you are serving do not have to get meals for teachers, and these things when the children are sent away, those who are in the schools are going on with education. Those who come back after a week or two it very difficult to catch up. Also the classrooms are crowded because we lack teachers and yet we have teacher training schools, we have teachers who are unemployed at the moment, and if we are earning (inaudible) so really, when you come to the sickness, we have more hospitals now than we used to have during the colonial days. Nambale Constituency never had a hospital during colonial days until towards independence when we had Nambale health center here. Our nearest hospital was Kakamega, we have many more hospitals around, but they are useless to be here at the moment because there is no medicine, the staff there are underworked or overworked, they have no morale to work and you find eventually you get surprised to read that medicines have been destroyed because they have expired. We keep on getting this donors, bringing in money, bringing in medicines na wananchi wanakufa kwa sababu hakuna madawa kwa hospitali, ukienda kwa hospitali unaambiwa nunua shidano, nunua kila kitu, unanunua madawa hata kupigwa shindano na yule daktari au nurse ambaye yuke kwa hospitali ya serikali unakuwa charged 20, 30, 50 Kshs, ili upigwe shindano na huyo daktari analipwa. So tunafanya watu kuogopa kuenda kwa hospitali, kwa hivyo wengi wanakufa kwa kukosa pesa za kuenda kwa hospitali ya private hospital. Hospitali zetu za serikali hazina maana sasa.

Ukiangalia mambo ya umaskini there poor kuna watu wengi ambao wapetupwa nje ya kazi, kwa sababu zisizo sawa, hiki kitu wanaita retrenchment Ok, World Bank na IMF wanafanya mipango, zinaambia serikali mnasema tutatupa watu nje sisi tutawapatia pesa ya kulipa hawa. Juzi hata American Ambassador ambaye alienda akasema kila mtu ambaye alikuwa ametupwa nje kwa sababu ya retrenchment hanastahili kupewa shillingi 200,000/40,000. Wale watu ambao walitolewa nje the maximum they have had ni shilling 40,000, sasa hii 200,000 hata serikali yenyewe haijawahi kuambia watu hizi ziko wapi, na tuliambiwa ziko. Na hiyo iko kwa Constitution na Constitution haifai. Ile kitu ningesema ni kwamba kwa sababu ya mtido huu, umaskini umeingia, watu wengi wametupwa nje ya kazi, walikuwa wamezoea maisha fulani hawawezi kuhudumia familia, sasa wizi umeingia, kuna watoto ambao wamesoma wanakuwa graduates hawana kazi, lazima wajue vile watajilinda, na hiyo ndio inaleta hii mambo ya kuwa na ufisadi, kuwa na mambo mengine, kuwa na wizi na unyang'anyi na mambo mengineo. Kwa hivyo ingekuwa vizuri kama for example hii mambo kwenda kwa shule harambees ndizo zinaumiza watu. Harambees zikatwe ziwe ni za kusaidia mgonjwa kwa maana ugonjwa hutarajii hiyo, ziwe niza kusaidia mtoto kuenda ng'ambo, ziwe ni za kusaidia maskini ambaye amekufiwa, lakini zisiwe za shule ambazo hata wengine wamejenga shule nzuri na harambee bado sinaendelea, zingine harambee zinaendelea kwa mashule kwa miaka na miaka, ukienda huko hakuna shule mpya ambayo inajengwa na watu wangali wanaendelea kulipa harambee. Haya mambo yachunguzwe, na harambee zingine hata zinaenda kuwa personal Permanent

secretary akikufa au Minister amekufa harambee inatolewa ya million mbili mwananchi anakufa huko anazikwa kama kuku tu au kama mbwa. So, ziwe harmonized na tufuate harambee ambayo tuna hakika itaenda kufaidi wananchi. Kufuatana na hayo mimi niko recommendations chache za kufanya ambazo nafikiria ni muhimu sana. Watu wengi wamefanya hizi recommendations na hii ni recommendation ya sasa mamlaka ya wale watu ambao wanastahili kuwa kulinda sisi wananchi.

Post ya President instahili kuwa Executive President kwa maana awe elected by the people. President ambaye anachaguliwa na Bunge, Bunge itaenda kumng'oa kesho na wakitaka afuate ile wanataka na asipofuata wana mng'oa na itakuwa unstable, President pia ataogopa kutekeleza mambo yake kama President, kwa hivyo awe Executive President na awe na powers za kutosha ili awe, anaangaliwa kama mkubwa wa nchi au the God the father of the Nation sio huyu President ambaye tutakuwa tunamtupa tu kando, na kando kwa maana tumeng'oa mamlaka yote, kutoka kwa President. Na President awe anafutwa na wananchi, kwa maana akiwa ni President ambayehakupigiwa kura, wale ambao walimchagua by selection watamtupa ten times, na mwananchi hata hatajua ni nini inaendelea na kwa hivyo President anastihili kuwa elected na wananchi na afutwe na wananchi na apewe Executive powers. Anstahili kuwa na Vice President na tuwe na Prime Minister, na huyu Prime Minister awe ndiye anasimamia mambo mengi ya serikali let them share the powers. Na Prime Minister naye awe na labda wasaidizi kama watatu kuwe first deputy Prime Minister, second deputy Prime Minister, third deputy Prime Minister, after all hao watu nao wachaguliwe na President kwa maana Prime Minister is just a Minister except he is the head of other Ministers, na Minister wengine tunanyamaza tu, kwa hivyo President achague hawa watu wote, lakini awapeleke kwa Bunge, Bunge I-confirm, ikikataa mmoja waseme huyo hatumtaki leta mwingine tumchunguze.

Interjection Com.Nunow: Please summarise.

I am nearly through asante. Inginge inastahili tuwe tuko na National Assembly yaani Parliament, ni vizuri tuwe na senate, na hii senate iwe na watu ambao wamekomaa ambao hawako chini ya miaka 45. Na hii senate labda kila District iwe na Senator mmoja, hawa ma-senators wawe wanaweza kuuenda kuchungua mambo ya Bunge, ambayo Bunge inafanya, hivi juzi Mbunge anakaa, wa-Bunge wanakaa wanapitisha mishahara yao, wanapitisha hii, hata hawa-consult nchi na hakuna mtu ambaye aliweza kusema basi kwa sababu wanafuata sheria, na hii sheria kuangaliwa isipoangaliwa itakuwa matatizo kwa hivyo I recommend ya kwamba senate iweko.

Local Government: Tuwe na local government ambayo ini strong, iwe kama County na hiyo local government wale watu wa local government ma councilors wapewe uhuru wa ku learn hizo local government zao, Minister wa Local Government kukaa na kusema nime-abolish hii local council kwa sababu ya fitina. Local Council ku-abolish au kugeuza kuweka Commission iwe kama ma-Councilors 51% ya ma councilors wa Tume ya kwamba wanataka local government, igeuzwe au at least one third ya population yaani electors ndio wageuze mambo ya local government. Kwa maana the local government zimeachwa tu at the wimps of the Minister for Local Government na hao hawapatii nguvu ma councilors kuendesha kazi vile wanastahili kuendesha.

Lingine, hii mambo ya majimbo nafikiri is a good idea, lakine iwe tu Provincial waweke majimbo Provincial kwa Constitution na iwekwe peding for 15 years to come ili kutakuwa hizo na election tatu ambazo zinafuata, wale ambao watakuwa huko, hawa vijana kama hawatakuwa integrated enough wakifikiria it is important kuwa na majimbo waletu, kwa sababu kwa sasa kufuatana na vile tulivyo economically, tutakuwa tunaumiza wananchi kuleta majimbo saa hii, but it is a good idea to have hiyo majimbo.

The other thing, referendum nafikiri ile Constitution ya Lancaster kulikuwa na referendum na hiyo ikatolewa. Referendum isiporudishwa, hata hii kazi nyinyi ma-commissioners mnafanya ni bure, kwa maana wa-bunge wakisha ingia kwa Bunge wategeuze hii kazi ambayo mnafanya, mmechukua nafasi ya kuifanya mmeifanya kwa ustadi, na hiyo inaweza kugeuzwa within 30 minutes. Hii section 2A iliingizwa within 15 minutes, section 2A tuliitoa mini nilikuwa Mbunge kwa 30 minutes na hii Coinstitution watu wanaichezea tu namna hiyo, kwa hivyo iwe na referendum wananchi waangalie na hiyo referendum labda ichukwe 75% of wananchi ambao eligible voters, kusema ndio ili wategeuze, kwa maana hiyo pia itakuwa inafanya wananchi kukaa bila yale mambo mengine kutolewa tu behind the kitchen Cabinet wanaharibu nafikiri hiyo ni very important.

Wazee wengine wamesema juu ya hii local brew, during colonial times mwafrika alikuwa hakubaliwa kunywa pombe ya wazungu walikuwa confined kwa ile pombe yao ya kiafrika, saa hii mwafrika amekuja amegeuzwa mtindo, anataka mwafrika akunywe pombe ya mzungu peke yake asinywe pombe yake mwenyewe. Kwa hivyo na hiki kitu kimeleta corruption nyingi imefanya wananchi kuwa maskini kwa sababu kama wangekubaliwa vile wengine walisema hapa wakunywe, wanajua kutengeneza pombe yao ya kiafrika ya wimbi na nini which is a food as well as a drink, ni chakula kama angekubaliwa kutengeneza. Saa hii kwa sababu ya restriction watu wengi wamekufa kwa sababu ya drinking illicit drinks, wamekufa kushinda siku zile kama hizi drinks zilikuwa zimekubaliwa. Kwa hivyo wananchi wapewe ruhusa ya kutengeneza pombe yao.

Jonathan: Ne bienyekhana ni ya khurula musikuli arare imali mungu na aba arula musikuli naye omundu omusiani undu amubachirisia na amubukula saa

Translator: Inatakikana akimaliza shule alete mali nyumbani, lakini inaonekana akimaliza shule kijana mwingine anajitokeza tu anamnyakua.

Interjection Com.Ayonga: ngoja mnyamaze. Mzee tunaelewa, ukachukua mali na ukasomesha msichana, halafu msichana wako alimaliza shule, halafu amekutana na kijana town, kijana amemchukua kwa hivyo unataka nini?

Jonathan: Nyenye ikhwe, amala mika ekhumi nasiri khurera ikhwe khaba

Translator: Anataka mahari, kwa vile wasichana wanamaliza miaka kumi without kulipiwa mahari.

Jonathan: Eliakhubiri omundu akhola emirimo ni yakhamala khurula musikarai niyakha-retire ne khandi yetsa mirimo kia county council kicha khandi yesi yenye khweyandikishamo

Translator: La pili, mtu anafanya kazi ya serikali amalize a-retire na akikuja hapa nyumbani hata ya county council likitokea yeye pia amo humo ndani hawajui hawa wengine.

Jonathan: Elia khudaru osomesha omwana asome khalala mukilasi ndala nende musungu nende omuyindi nebasome mukilasi ndala nemiremo kilaba kinyolekha nebabukula omusungu ne balekha mumali uno khulwakhubere nemumali nokho

Translator: anasema kuwa watoto wanaweza kusoma pamoja na wazungu na wahidi kwa darasa moja na wamalize sawa sawa, lakini kazi ikitokea mzungu ndio anakuwa preferred au mhindi, na huyu mwafrika anabaguliwa kwa nini?

Jonathan: Yangu ni hayo

Com.Ayonga: Asantemzee yule anayemfuata, wale ambao nimewaita ningetaka msonge hapa na mfuatane James Ekesa

James Ekesa: Asante sana, nina mawazo yangu, kwa majina ni James Ekesa Vilema. La kwanza rumand, mtu anashikwa anapelekwa rumand kwa miaka tano sasa kifungo kitakuwa miaka ngapi?

Interjection Com.Ayonga: na usituulize maswali sikiza huwezi kutuuliza sasa unataka kutuambia tufanye nini?

James: Kama hiyo ni sheria itolewe, kama ni makosa itolewe kama ni sheria ambayo ilikuwa inaadikwa.....

La pili, kuna Province mbili tu katika Kenya nzima ambazo infaidika na kazi kama factory au TTC au kitu ingine, lakini sisi watu wa Western hatuna chochote sijui sisi tuko Kenya wapi. Tunataka pia kila Province iwe ikipata kitu kuliko Province mbili peke yake katika Kenya nzima. Nairobi Province na Coast Province.

La tatu, nafikiri la mwisho lilikuwa kwisha semwa, ya kwamba mtu akistaafu anapewa tena kazi ingine, si vizuri mtu kupewa kazi ili aende tu afungue kazi na aajiri watu wengine wale ambao walikuwa nyumbani kuliko tena kupewa kazi ingine ya madaraka serikalini. Asante sana.

Com.Ayonga Jafas Wadera, ndiye huyo, Selestino Oteba, Selestino yuko? Kuja karibu halafu Okemo Saferio, Okemo Saferio, uko hapo. Sasa wewe karibu jinsi ambavyo nimeita majina mwanfuatana namna hivyo, halafu kuna Michael Nangira, Michael Nangira yuko. Basi mnanfuatana namna hiyo.

James Wandera: Asante Commissioners na wanao husika. Mimi langu nitaongea juu ya umaskini ambao umekumba nchi

yetu ya Kenya. Nilikuwa napendekeza ya kwamba, katika Katiba, ingekubaliwa ya kwamba, kila mwananchi wa Kenya ambaye huwa anahesabiwa maana yeye ni mtu mzima na anajulikana, kama kwa mfano saa hii, katika nchi ya Kenya inajulikana ya kwamba, tuko watu milioni 33 na umaskini umekumba nchi yetu. Kwa hivyo nilikuwa napendekeza ya kwamba kama inaweza kupitishwa kama sheria kila baada ya miaka mitano wakati wa uchaguzi, kila mtu mzima huwa anahesabiwa, awe akipewa shilingi kama million 1 kwa kila kipindi cha miaka mitano inapopita, ili ya kwamba iweze kusaidia kupunguza umaskini kwa sababu wale ambao watukuwa bado hawajapata kazi, wanaweza kuanza kujimudu na hiyo million moja, wale pia ambao hawewezi kusomesha watoto, maana hawana kazi, wanaweza pia kujimudu pia kwa hizo pesa,

Interjection Com.Ayonga: umesema watu wapewe million moja in five years, ni maoni yako? Toa maoni mengine.

Jafas: hilo ndio nilikuwa naona ya kwamba ni la muhimu kwa sababu kuna hiyo itakuwa ni njia moja ama pendekezo la kupunguza umaskini kwa wale ambao hawajiwezi. Million moja kwa yule ambaye amesabiliwa.

Com.Ayonga: Jiandikishe kule, next Selistino

Selistino Oteba: Asante ma Commissioners, nitachukua wakati mfupi kwa maana mengi yamezungmzwa Selestino Oteba Munyekenye. Maoni yangu ya kwanza ni kwamba nominated MPs should not be appointed as Cabinet Ministers.

Ya pili nasema those who plunder the economy of the country should be barred by the Constitution of this country to vie for any political seat. Their property should be consphicated to recover the money. I think they should be taken to court. My next point Commissioners is that the Members of the Executive should not interfere in the work of other arms of the government, or they should influence decisions of other arms of the government. My last view is the distribution of the National cake, should be equal. Thank you.

Com.Ayonga: where is Mr. Okemo?

Okemo Zabelio: Mimi kwa majina naitwa Okemo Zabelio Okemo. Nimzaliwa wa hapa Buhaya. Mimi naomba hii Commission hii, kwa maoni yangu mimi naona hafadhali iweke sheria, mtu hapa ni Buhayo na ukitoka nje hata kama wewe ni kabila gani umeingia Buhayo, fuata sheria ya wanaokaa Buhayo. Na kitu kingine, kuna makabila mengine hapa wanaojipenda sana kusifu ukoo wao, wakikaa pale watu watatu, wanataja ukoo wao, na wanawacha ile jina ambayo wa Hayo waliweka. Na kama mnaweza kunikubalia nisema huo ukoo ambao inapendelea hivyo naweza nikasema.

Com.Ayonga: Nataka kusema hivi, hatukuja hapa kwa kuwasha moto, na hatutaji mtu yeyote, kama kuna tabia ingine ambayo watu wengine hawapendi nasema kuna tabia fulani ambayo pengine tusingependa lakini isije iwe kwamba, ile nyumba fulani ile, ile nyumba fulani hiyo, huo nikuengeza uchochezi na kuwasha moto ambao hatutaki. Na ninataka nyinyi mnyamaze

huko nyuma mimi ndie nina-deal na huyu mzee. Kwa hiyo mzee uendelee nataka unipe point yako ya mwisho. Hiyo tumesikia, wengine hujipenda na kweli si hapa tu, hata huko kwetu Kisii wako wengine.

Okemo: Neno la pili, watu ambao wanaajiriwa na serikali kuanzia waalimu, ma-chief, wote tunataka wapate transfer kwa sababu sisi wananchi bado hatujawachagua, serikali iliwachagua, ni watimize sheria kama ile, ile inashika DO na ya DC, hawa pia wafuate sheria kama hiyo.

La tatu, sisi hapa Nambale au tuseme Busia tunashida kubwa sana, Mungu aligawia watu mimea ambayo inaweza kuwapatia watu wao mapato, na kila kitu. Tunashangaa sana sisi kuambiwa hapa tulime miwa na serikali yetu inanyakuwa factory yetu inakuja hapa inapeleka Kericho. Sasa sisi hapa miwa yetu tutapeleka Kericho au wapi? Tunataka factory kufuatana na miwa ambayo tumelima ni mingi. Asante.

Com.Ayonga: Wapi Michael Nangira? Micheal Nangira: Kwa majina ni Micheal Nangira kutoka Elwahana village Biwok sub-location Buhayo East. Nina mapendekezo ya fuatayo, kwanza, Wilaya ambazo zilitengwa na zina majina ya kikabila kama vile Teso, kama vile Nandi, kama vile Kisii, Turkana, ningependa, hayo majina yafutwe na majina mengine ambayo yanaweza kutusaidia kuwa na umoja wa kitaifa yakwe kwa mfano badala ya Teso, tutumie jina kama vile Amagoro, badala ya Turkana tutumie jina kama Lodwar ndio tusiwe na ukabila. Kisii kama kuna mti huko ambao unaweza tumiwa, huko Kisii nadhani kuna miti.

Pendekezo la pili, upande wa University Admission kuna body ambayo inaitwa joint admissions board. Hii board huwa inaamulia mwanafunzi kufanya faculty ama profession ambayo pengine hakupenda, kwa hivyo ningependa mwanafunzi aachiwe kufanya ile profession ambayo amechagua yeye mwenyewe, sio kuamuliwa. La mwisho ningependa hawa Ministers wote ambao wanateuliwa wapitie kwanza through vetting kwa Parliament ndio wakuwe Ministers. Asanteni.

Com. Ayonga: Kuna Moses Sauke au Sauke, ndiye huyo? Halafu Lawrence Ilude, Lawrence yuko; na huyo Fredrick Matini, yuko? Silas Alabi yuko? sasa endelea, niliwaambia wa Luhya wanabarikiwa na mvua fanya haraka ili na wengine tuwasikize.

Moses Sauke: Kwa majina naitwa Moses Sauke, na I propose pension kwa civil servants isiweko na instead wapewe final dues, and not pension. Halafu retirement age iwe at least 45 years of age. Pia Presidential election to be a President I propose you must not also be a member of Parliament, instead people should elect a President who is not a Member of Parliament. I would also comment on prosecution process. On prosecution process, an accused person should at least be given a chance to defend himself before the hearing continues, because at present somebody is accused and wait for the proceedings to go ahead then he is only given the last time to defend himself. I oppose the prosecution process which is their now.

Lastly the present land ownership rights especially the succession process you see this lands are always divided divided I

propose the government to take over the land, and because it lowers the population of the country to at least suggest and live the Provincial Administration to decide on how to share the land, and give extra land to fellows who do not have, especially the street fellows, and those who have are born out of wedlock, then the division or the share, the government should give at least approximate of 10 acres to somebody who is unemployed, to practice his employment on the farm. That is all what I have.

Com.Ayonga: Kuna huyu Isaack Sidialo, lakini wewe ulipokuwa unasema kwamba, watu wasipewe pension, yako imekuwa ni original kabisa, hakuna mtu amesha tuambia hiyo Kenya nzima, kwamba watu wasipewe pension, ni wewe tu.

Isaack Sidio Okwara: Kwa majina ni Isaack Sidialo Okwara, nikiwakilisha vijana wa Bwilare sub-location kutoka kata ya Walaji. Ningependa tu kusema mambo mawili, matatu na niache. La kwanza, ni kufuatana na uchaguzi wa ma-Mayor na wenyekiti wa mabaraza. Jambo hili kama vijana wa Bwilare wanapendekeza kwamba, wawe wakichaguliwa moja, kwa moja na wananchi, kwa sababu wananchi ndio wanajua na wanaona huduma ambayo wanapata kutoka kwa ma baraza, kwa hivyo mambo ya kuchaguliwa na ma Councilor sio vizuri na wanatoa huduma iliyo duni zaidi.

Jambo la pili nitaongea kuhusu kuridhi mashamba. Mashamba inakuwa ni shida sana kwa vijana, unapata kupata cheti cha shamba kama title deed, au number ya shamba, inachukua mda mrefu na inagharimu zaidi kwa hivyo vijana wengi, hawawezi hata ku afford malipo ili kubadirisha mashamba kutoka kwa wazazi wao. Kwa hivyo tunataka hali ya kubadirisha mashamba, irahisishwe, malipo yawe kidogo, na hiyo huduma iletwe chini, hadi hata katika kata. Kwa hivyo Liguru na assistant chief na chief wanajua mtu ambaye amezaliwa pale, wazazi wake, na wanaweza kuwa mashahidi kufuatana na huyo mtu anavyotakikana aridhi lile shamba.

Jambo lingine ni mahali pa Rais kuwa na mamlaka, Rais ana mamalaka zaidi, anateua hata watu wasiokuwa na ujuzi kikazi, kwa hivyo tunaona hafadhali wawachie Bunge liwe likichagua, watu kama ma-Commissioners, na wenye kiti wa mashirika mbali, mbali na iwe wanaangalia ujuzi wao, masomo yao, wakaguliwe wapewe interview na wachukuliwe kufuatana na vile wamesoma.

Point ya mwisho serikali inatakikana tuwe na Waziri Mkuu ambaye anachaguliwa kutoka kwa wabunge walio wengi. Nashukuru.

Com.Ayonga: Harun Ombaso, Harun Ombaso ndiye huyo, halafu Dickson Masika. Dickson Anaseti Odongo. Harrison Opemi ameenda. Kwa hiyo endelea Ombaso.

Harun Ombaso: Thank you Mr. Chairman, My names are Harun Ombaso Matoko. I represent (inaudible) youth self help group. My first point is that, corporation among East African countries, i.e Kenya Uganda and Tanzania, there should be an

official one Identity card that can make different citizens to travel around without harassment from custom officials.

Secondly is about bursary funds. Bursary funds should be issued equally there should be no discrimination, whereby bursary fund goes to when it kicks off, and poor people go all suffering.

Third point is that town councilors, this is based on town councilors Taxation of business men and women should be put off or payment should be affordable to those once who can do with it. Lastly, that is the fourth, loans for agricultural farmers i.e. whereby you have got bodies such as agricultural farmers corporation, they should actually help farmers to motivate their agricultural products and get a wide market whereby they can move on with their lives well. I do not have much that is all I have. Thank you.

Com. Ayonga: Obanda.

Obada Ouma: Majina ni Obada Ouma, niko na mapendekezo machache ya kufanya. Ya kwanza kabisa nitaongea kuhusu uraia. Mtoto ambaye wazazi wote wao ni wazaliwa wa Kenya, wapewe uraia bila swali. Mtoto yeyote anayezaliwa na babake awe mkenya apewe uraia. Mtoto ambaye anazaliwa na mama yake ni Mkenya na babake si Mkenya, apewe mda kwanza ndipo maombi yake yafikiriwe kama mzaliwa wa Kenya.

La pili Rais, Rais asiwe mbunge, achaguliwe na 25% kutoka kwa Province tano. Raisi kabla ya kugombea kiti cha Urais atangaze mali yake na jinsi alivyoipata.

Ya tatu ulinzi wa taifa, Rais asiwe amri jeshi mkuu wa taifa la Kenya. Ni hayo tu.

Hiyo iwachiwe waziri fulani ambaye atateuliwa na Bunge.

Com. Ayonga: kuna Peter Ouma lakini nimeona jina hili Peter mara nyinga sana.

Huyu Peter nadhani tumefanya kuna Osiato, Osiato kuja hapa mbele, na Paula Kapo Ndubi, niliona hili jina ndubi ni lingi ni hapa na nilidhani wa Kisii walihama kuja hapa?

Au ni wale tuliwacha nyuma. Bonson Osiato

Bonson Osiato: Commissioners, haya ndio yangu ambayo naweza kusema. Kwa majina naitwa Bonson Osiato mimi naona kwamba wakati wa kupiga kura, wasipige kura siku moja ya councilor, mjumbe pamoja na ya President. Tuwe na system ambayo kila kura inapigwa siku yake.

Ya pili registration of societies, tuseme especially kanisa, kuna mpango ambao registrar general ningependa watengeneza, Commission ione kwamba tuanzie grassroots ndio kanisa iwe registered kwa sababu hawa kazi yao ni ku-collect shilling 1,000

kwa kila kikundi ambacho inataka kuwa registered, na mwisho you are rejected kwa sababu, makanisa makubwa kama Catholic na Anglican ndio wako huko juu.

Ya tatu, sioni kwa sababu Kenya ni maskini tutafute wataalamu iwe medically, awe iwe sheria kwamba wataalamu kwa kuandika Katiba watoke nje. Tuna wadugu ambao wamesoma hapa Kenya.

Ya nne, ile ambayo imesemwa sitarudia ijapokuwa Police wame-benefit vitu sana kutoka kwa chang'aa na busaa, ndio sababu hata police hawawaulize serikali kuwaongeza mshahara, akitoka tu amepata chumvi. Ya mwisho ni kwamba local authority especially Municipalities or the city council kama ile ya Nairobi, raia maskini hana nafasi ya kuenda choo kwa sababu vyoo vyote vimepewa chokora. Shillingi mbili, shillingi tano, shillingi kumi. Raia akianza kukaa vizur iserikali iangalie ndani ili vyoo viwe kama vile vya zamani, vile ambavyo vinawachiwa municipality yenyewe kuliko kupeana kwa chokora.

Ya mwisho ambayo naomba tu, ni kidogo kwamba ningependa sisi wakati tukisoma historia wakati wazungu waliingia hapa walikuja wakapata sisi tulikuwa na watawala kama Kabaka, kama hama tulikuwa na Mumia, nataka ile system irudi na tuwe na hii election ikomee kwa Prime Minister na tuwe na supreme court, kwa sababu neno President imefanya karibu kila mwenda wa zimu anataka kuwa President. Asante sana.

Com.Ayonga: Walter Manyasa, Chrispine Okedi? hakuna, Wabwire Simpriosis, Africanis Guluma, sasa tunaingia majina magumu kabisa, ndio ya kumalizia, malizia, Patrick Buluma ndie huyo na huyu Florencio, wanaume wanaitwa Florencio? wewe endelea.

Patrick Buluma: Hamjambo sana ma-Commissioners kwa majina naitwa Patrick Buluma Odilo, mimi nimzaliwa wa sehemu hii. Yale ningependekeza tu kwa hii Commission ni kwamba kuna sheria ambazo zimepitwa na wakati na nita quote tu hapa mbili, hasa tukienda upande wa mahakama utakuta mtu akifungwa mzee wa miaka kama sabini anapatikana na makosa, anafungwa miaka tano, anapewa tena adabu ya kuchapwa viboko, hiyo ni sheria ambayoi kwa maoni yangu ningependekeza kwa hii Commission ya kwamba imepitwa na wakati na sheria kama hiyo, inatakikana iondolewe, pia sheria kama ile ya kunyonga. Tunajua ya kwamba ni Mungu tu anayepeana uhai hakuna binadamu anayejua ya kwamba hakika mtu fulani alifanya hilo jambo. Ninataka ya kwamba sheria kama hiyo ya kunyonga iondolewe katika Katiba ya Kenya, na mtu afungwe kama ni kufungwa, afungwe kifungo kirefu lakini asinyongwe.

Point ingine ambayo ninaonelea napendekeza ya kwamba wabunge wetu wamejipatia (inaudible) kwa kujiongezea mishara, tuna sahai maskini wetu ambao ni watu wasiojiweza, viwete, na watoto wengine mayatima. Ninaona ya kwamba mda ambao walipewa mda ule wa miaka mitano ni mrefu sana. Naona ya kwamba huo mda upunguzwe, tuwe na kipindi cha kukaa kwa bunge, kura iwe ikifanyika kila baada ya miaka mine, tusiende mpaka miaka mitano.

Jambo lingine la kumalizia nasema ya kwamba, kwa upande kama wa federal system of government tumeona ya kwamba mpango kama huo umeanguka katika nchi zingine, kwa hivyo siupendekezi katika jamhuri ya Kenya kwa sababu unaleta ukabila na unaleta kutoelewana, we want a unitary government. Asante sana.

Com.Ayonga: Fredrick Nabongo, ndiye huyo, Kizino Ladoli, amekwenda, Elkanah Wekiu, ndio wewe mzee bona unaogopa jina lako Hezron Omuruoni, ameenda, Fredrick Ongelo yuko, hayuko alikimbia mvua. Basi tuendelee na wewe, sema majina yako.

Fredrick Nabongo: Majina yangu ni Fredrick Nabongo, na ninaenda kusema haya, nitachangia kuhusu makinisa. Ningependelea kusema ya kuwa sheria ambayo iko Kenya ya ma-kanisa yaani kuabudu kuwa huru kwa kila mtu, ingegeuzwa kwa ajili wakati huu tuna makanisa ambayo hata watu wanamuabudu shetani. Na hii ikiwa inaweza kugeuzwa, kanisa linapokuwa linaadikishwa hapa Kenya, na wanaanza kumuabudu Mungu, serikali ingefaa kufuatilia na kuona set up ya Kanisa hii ni namna gani, Ili kila kanisa likaweza kuwa na Constitution yake. Na iweze kusomwa na serikali na hata area ambayo kanisa lile liko liweze kueleweka vizuri ili tusiwe na mikasa ya kuabudu shetani, jambo kama hili wa Kenya wengi hata wamesikia kunakuabudu shetani. Na inakuja kwa ajili watu wamekwa huru kuabudu Mungu jinsi wanavyotaka, sasa watu wameacha kuabudu Mungu kwa njia nzuri wameanza kuabudu kivyao. Tunafaa hiyo sheria ichunguzwe na weweze kufuatilia.

Jambo lingine ni ndoa, ndoa ni jambo ambalo Mungu mwenyewe aliweza kuanzisha kwa hivyo watu wanapoona, serikali ingefaa kuweka sio upande wa kijana ama wa kike, tunaweza kuwa na mtu amesoma kutoka kwa pande hizi mbili, mmoja wao sasa utaona mmoja anapotaka kijana pengine anataka kuoia msichana familia ile ya msichana inaona huyu kijana hafai kufanya nini? kuoia pale lakini Mungu mwenyewe aliweka ndoa ni upendo, watu wakiwa wamependana, watu wale waweze yani kupata kuoana isiwe ndoa ichukuliwe kama commercial dealing kwa maana iwekwe ndoa iwe jambo la upendo na ionekane ya kuwa, kile kitu ambacho kijana atatoa ionekane tu ni kupigia familia ile asante. Kijana huyu anaweza kuwa pengine

Com.Ayonga: wacha story.

Fredrick: Point ingine ninaenda kwa corruption, jambo corruption lina kuja hapa nchini mwetu kwa ajili sisi wananchi wenyewe tunachangia corruption kwa njia hii. Mimi ninapo shikwa ni jambo nzuri kama tunaweza kutetea sheria, ninaposhikwa na police, watu wangu wakuje kortini na waone vile jinsi korti itaamua kuliko kupea askari pesa.

Jambo lingine ni kuhusu mamlaka ya Rais, mimi ningependekeza hivi, Rais wa Kenya inafaa achaguliwe na kila mtu na tusiangalie jama, anatoka chama gani, vyama vyote ni vyetu hapa Kenya na tunafaa tu kuchagua mtu kulingana na uwezo wake. Asanteni.

Com.Ayonga: Nataka ujue makanisa yote yana Constitution yao, hakuna kanisa ambalo linakuwa registered na registrar of societies bila ya kutoa Constitution. Nimetaka tu kukuhakikishia uje hilo. No I am telling you just a mere fact I do need any support thank you thank you. Enda ujiandikishe I do not need any support because it's a matter of fact.

Elikanah Vikiru: Mimi majina yangu ni Elikanah Vikiru na maoni yangu kuhusu Katiba hii ninaona ya kwamba tumesikia wakati mmoja wakisema ya kwamba tunataka serikali ya majimbo. Mimi maoni yangu ninaona ya kwamba, serikali za majimbo niza kikabila. Kwa sababu tunaweza kuwa na mtoto kutoka hapa Western, hawezi kufanya kazi Mombasa, hawezi kufanya Nairobi, atafanya Western. Na ikiwa Western peke yake, hiyo ni kama ukabila. Hata mtu anaweza kutoka upande wa Mombasa, anaweza kutoka upande wa Eastern afanye kazi hapa, sasa mimi nataka serikali ya majimbo isiweko, tuwe na serikali kama hii tulio nayo, mwananchi atembe mahali popote katika Kenya.

Ya pili ninazungumzia habari ya mtu ambaye ana mke wake na ana mali yake, na ana watoto wake. Wakati mmoja bwana anaweza kufa, na bwana anapokufa ndugu ya huyu bwana, wanakuja wanyang'anya huyu mwanamke, ambaye bwana ndugu yao amemuacha, wanamnyang'anya vitu, wanasema vitu vya watoto wetu, vitu vya ndugu yetu, na huyu mke amewachwa na watoto, mimi naona ikiwa mume amekufa na wamefanya ndoa na mke wake mali hiyo mke apate kuridhi na atunze watoto, watoto wakisha kuwa wakubwa huyu mke apate kugawia watoto hawa urithi wa baba yao.

Ya tatu, nikuhusu habari ya gereza zetu za Kenya ambazo zinatakikana watu wanaofungwa katika Jela, wanafungwa kama wanyama, hata wanyama wako afadhali. Mahali wanapolala, wana lala kwa sakafu. Pale kwa sakafu hakuna blanket, mtu huyu mahali pale, chakula ambacho wanakula, chakula kile hata si chakula cha binadamu anaweza kula, chakula kile kinapikwa ugali maji, maji na anapewa tawi moja la sukuma wiki, ili apate kula. Na hii si haki ya binadamu, inatakikana serikali ijue ya kwamba, mtu huyu amefungwa kwa makosa fulani ili na inatakikana anapoingia katika gereza ile aende afundishwe nidhamu na afundishwe mambo fulani, akitoka kule awe amebadilisha mawazo yake, ikiwa amejifunza kule ufundi, au ujenzi, anaporudi nyumbani abadilishe nia aanze kufanya kazi ile ambayo amefundishwa kule, na imletee mapato asiwe mhalifu. Hilo ni neno ambalo ninaona katika gereza zetu, unaweza kuona ndani ya gereza ile, watu wanapangwa saa za jioni, wanapangwa kama miti, huyu kichwa, namna hiyo kwa hivyo tunataka watu wale watunzwe wapewe mahali pa kulala pazuri, chakula kizuri kama binadamu.

Com.Ayonga: sasa nimesahau dakika yangu moja na nusu na hamtaki kunisaidia. John Momanyi au mlimai, yuko? Hayuko, Hosea Mlongo, Hosea Mlongo, Shaban Wandera, Halafu kuna Labat Wanga, unaona giza imeanza kuingia hapa, kuna Lukas Virunga Kokonya, uje mbele halafu kuna Wandera Wilfred, Wandera Wilfred yuko? Hayuko, Oluoch Ochieng, halafu kuna godfrey bwire.

Lukas Virunga Kokonya: Kwa majina naitwa Lukas Virunga Kokonya, nitaanza na youth. Youth tuko na shida ya kazi, mimi youth ningependekeza kwa hii Commission ikuwe mzee kama wewe umefanya kwa serikali ama bado unafanya kwa

serikali vile unafanya hivi, mtoto wako asipewe kazi na mtoto wa yule ambaye amesoma amemaliza, hajapewe kazi wako apewe kazi, na yule wa maskini akae, pendekezo langu la kwanza.

La pili, niko kwa wasichana youth nasema hivi, msichana anaweza kuja na mama yake, mtoto wa kambo sio kuwa akuwe na haki ya kupewa uridhi kama mzee wake amekufa kuwa apate mali yangu, na amekuja na mamake, wakati alikuwa anapewa mali anarudi kwa baba yake. Hilo ni upande wa wasichana. Upande wa wanaume iwe kijana wangu akipeana mimba kwa msichana wako, iwe wote sisi wawili kama ni kufungwa, vifungo, tufungwe sisi wote sio kijana ndio anafungwa halafu haya mambo ilikuwa ya kusikizana, kama rape case that is a different case. Tufungwe wote kwa sababu tulipendana ndio tukazaa.

Upande wa Provincial Administration ninoamba kuwa wa mama, mama yeyote kusema ati afanywe sub-chief, chief hapana, sababu ni hii Mimi ni bwana yake, mini pengine ni mnywaji wa pombe, natoka huko nimelewa na yeye tayari yeye ako na crown unapata ana ningojea na maaskari ananiweka ndani, sasa na yeye yuko kwa boma yangu sio kwao, sasa vitu kama hivyo mimi nakataa wa mama kuwa waakilishi wetu wa serikali.

La mwisho mzee ni hili upande wa tribalism, na hiyo ninasema hivi kufuatana na wajumbe wetu. Iwe Commissioners kama nyinyi tunawapa wa mama kwa mfano, hawasikii kiswahili ama hawaelewi Kiswahili vile ninaongea. Wawe sisi wananchi wenyewe sisi tunachukua uahayohapa, hapana kama wewe ulitoka sijui wapi, aa tunataka sisi wahayo nikizungumza kihayo, unawapa ambao hawasikii watasema kwa mfano, tunaka sisi Commissioners because once you are a Commissioner there is something sensitive within the government that you are now Commissioning. Hilo ndilo jambo langu la mwisho mzee asante.

Com.Ayonga: Kuna Alois Obias, Alois yuko?ameenda, kuna William Maina, William Maina, kuna Peter Okuku, Peter Okuku?ameenda, Solomon Njako ambaye ni Councillor yuko wapi? Ameenda,councilor naona umejianaa vilivyo, ninakupa dakika moja na nusu tu, tuambie maneno usisome hapo.

Councillor Solomon Njako: Asantesana bwana Commissioner kwa majina naitwa Solomon Injako nikiwa councilor. Mimi yangu sio mengi,ninataka kuguzia tu upande wa pension, ningependelea ya kwamba pension scheme iwe revised. Nina maana kwamba badala ya mtu akifa, pensioner for example akifa inakus yule mama ambaye amebaki kwa boma, a inherit hiyo pension kwa miaka mitano. Ningependa hiyo period iwe extended to 10 years kusudi mtu aweze ku-bring up that family.

Secondly on pension ningependa hivi, mama yule ambaye anaajiriwa na serikali na ana retire halafu akafiriki, bwana yake naye awe na uhuru wa ku inherit hiyo pension. Sababu gani? watoto wanabaki juu ya baba ndio atawa-bring up kwa hivyo tupewa nafasi kama hiyo both sides. Na Liguruus watu wamezungumza mambo ya Ligurus wapewe in service course, Liguruus wapewe in-service course na wapewe kitu kidogo kwa pay roll. Sababu hao ndio wanafanya kazi kwa grass roots. Hii post ya PC iwe scrapped off na ikuwe replaced by regional secretary ambaye atakuwa anapata records au information kutoka kwa ma-DC na anakuwa kwa Minister au kwa Permanent Secretary within that Ministry of Administration. Sababu mimi naona

kama iko duplication, PC from top hafanyi kazi yeye anafanya kazi ile ma-PC, ma chiefs ma assistant chiefs wamefanya, hio ndio pendekezo langu.

Interjection Com.Ayonga: Na kwa nini unapenda hiyo muwe na secretary ambaye anafanya (inaudible)

Councillor Solomon: They do not report directly until they come to confirm again on the ground. Secondly upande wa viwanda, mtu anafuga samaki hapa, au we grow fish for example in Busia District but we do not have a factory, kwa hivyo ningependekeza kwamba government injenge ma-factory na ma industry, mahali chakula kinapatikana, kwa mfano Thika wana-grow mananasi na kuna factory huko, sisi samaki yetu inatolewe kutoka hapa inapelekwa Nairobi for fish processing. Hiyo niaona kama tunanyang'anywa kazi kwa watoto wetu, na pia tunanyanga'nywa vitu vingi. Serikali itusaidie hapo. Mimi sitakuwa na mengi kwa sababu ya mda.

Com.Ayonga: Asante sana bwana Councilor, asante. Wilbar Wasirima, ebu kuja karibu, na Leonard Nyongesa, kuna mama hapa anaitwa Leornida? Huyu mama alikwenda. Vitalis Odhiambo yuko? Boaz Ofisi kuja hapa karibu, endelea.

Wilba Wanyonyi. Bwana Commissioner kwa jina ni Wilba Wanyonyo Wasrma makaaji wa hapa Nambale. Nina jambo tu kama mambo mawili. KBC mekuwa ni chombo cha kupazia habari kwa wananchi, lakini megeuzwa kuwa chombo cha kutoa kashfa kwa vyama na wanasiasa wa upande wa upinzani. Na kutoa sifa kwa chama tawala. Kama jana kipindi kilikuwemo muamko mpya, kama ungaliona hicho kipindi jana usiku kilikuwa tu kinatoa sifa mbaya kwa wanachama wa upinzani bila hata kusema neno angau moja ambalo mheshimiwa Oloo Aringo juu alisema ya chama kinachotawala. Kwa hivyo pendekezo kwa kuwa hiki ni chombo cha kupaaza habari kwa wananchi, kisipendeleo upande wowote. Na kiwe na uwezo wa kutoa elimu ya uraia, ili watu wajue civic education pasipo kuambiwa watu kutoa mambo ya bovu mkifanya hivi nchi yetu itakuwa kama Somalia, itakuwa kama Rwanda, itakuwa kama nini watu wanaogopa, mwisho ningesema mengi lakini yametajwa tayari, la mwisho ni Kenya imekuwa ni nchi ya watu wanao mcha mwenyezi Mungu, a God fearing state. Kuna mashule na hata Institutions ambazo tumetunikiwa majina ya watakatifu, kwa mfano kama Nambale Secondary school ni St. Thomas Nambale, Monica St, Mary's lakini wanaingiza majina ya watu wasio watakatifu, tuseme Monica Onyango, St.Mary's Onyango secondary Monica sasa watu wanakosa kuelewa huyu Onyango sasa amekuwa ni mume wa St. Mary. Hayo ni mapendekezo yangu.

Interjection Com. Ayonga: Hayo ni mambo ya kanisa katika utaratibu wa kanisa sio? Na tunaweza je kukataza kanisa kutofanya jinsi ipendavyo (inaudible) na faith ya watu wengine.

Wanyonyi: The church is over run I am saying this, nilikutana na kasisi fulani ambaye analalamika sana shule imepewa jina la mtakatifu kama St.Cecilia Nangina, tena imeingizwa jina la asiye mtakatifu huyu alikuwa ni kasisi, that shows that the church is over run. Kwa hivyo mimi ningependekeza hayo majina ambayo yamepewa mashule yametunikiwa na mashule ya watakatifu,

tafadhali wanasiasa, au viongozi wasiingilie wa kaweka majina yao, ndio tunaona sifa zimekuwa mbaya katika mashule yetu, hapo na mengi ambayo yamesemwa kwa hivyo ningependa nikomee hapo.

Com. Ayonga: Boaz Odipo ndiyo wewe,

Boaz Ofisi: Kwa majina yangu ni Boaz Ofisi kwa hivyo asanti sana kwa kupewa nafasi hii, Ofisi. Kitu changu cha kwanza ningependekeza katika Katiba ijao, President na Vice President wachaguliwe na wananchi directly. Na hiyo ndio naongezea na pia tuwe na Bunge mbili ambao representatives wa ile Bunge senate iwe waakilishi kutoka kila District. Ministers wawe wanachaguliwe na President ambao ndio wanachagua of commander in chief of the armed forces. Na Chancellor wa Universities apewe waziri wa education. Asiwe at President ndio tena Chancellor. Kitu kingine Ministers wawe vetted na Bunge, Ministers wawe vetted na hakuna kufutwa na President vile anataka. Wapewe nafasi asitolewe tu kwa vile President amependa, na ningependelea pia hao Ministers watoke kwa watu ambao wako na experience watu ambao wanaelewa na sio wale kutoka kwa Bunge. Cabinet Ministers wawe watu kutoka nje ya bunge, wa Bunge wawe tu wa bunge.

Pia ningesema upande wa land, Ningependelea hii Katiba iweko, kila mwananchi kila mwananchi ambaye ako na kipande chake cha land, apewe title deed, title deed iweko ndio corruption ambayo inaendelea kwa lands department iishe, kwa sababu hio inafanya vitu kama hivyo title deeds zinakuja za bandia. Lakini mtu akipewa land yake nafasi, title deed vitu kama hivyo ninafikiria itapunguza. Asante sana.

Com. Nunow: Asante sana, ningependa kuona wangapi wanata kuzungumza bado ambao wako katika hii hall. Ok.kwa sababu imekuwa giza, sitasema mambo ma dakika na mnataka mjitayarisha mind yenu namna hiyo. Kila mtu atakuja hapa aseme point moja peke yake. One point, not two if you want to repeat that was said its upto you but I will give you ngoja mzee bado nitaitana kwa list, bado nitatumia list lakini, keti tu tafadhali lakini nataka kila mtu kwa sababu hatutaki kuacha mtu yeyote, uje na point moja, kwa hivyo saa hii uwe unafikiria ni point gani muhimu sana ungependa kusema. Unakuja unasema majina yako, na unasema point moja na kusimama. So that is very clear na nitaanza na Kamilos Katere, is here there? Rev. Peter Okumu, Rev. Amos Lugalu, Rev. unataka kusema? Asante sana neno moja. Chukua neno tafadhali keep to one point.

Amos Lude Wamalwa: Kwa majina mimi naitwa Amos Lude Wamalwa, mimi ni Padre. Point yangu moja tu ni kufuatana na retire ya President. Nataka hiyo Katiba hii ipitize, President aki-retire arindwe vizuri na tena asiwe ati ndiye mwenye kiti wa chama chochote. Awachie President yule ambaye amechukua kuwa chairman wa kila kitu katika Kenya.

Com.Nunow: Asante sana, Rev. Jiadikisha tena kwamba umezungumza. Moses Obanya, yuko? Baraza Odugu yuko? Mwania John uko? Subiri kwanza nataka nifanye line up ili time isipotee, kuja hapa mbele, nikikuita unajua wewe ndio unafuata. Kujeni hapa subiri. Pandeas Okelo, Charles Nyangaro, Nyangoro? are your there,?Wilson Oboro Baraza? Kuja mbele, nyinyi wawili mje hapa mbele basi. Okay endelea.

John Muami: Asante mimi jina langu ni John Muami, niko na point kuhusu education act katika Constitution ya saa hii, ninapendekeza kwamba, shule za msingi Primary school should be run by the school committee. In the current school management, each school should have a school development plan which covers three years, but that school committee is elected after every one year. I propose that the school committee in a Primary school should also be elected after three years, so that they can work on that development plan.

Com.Nunow: Thank you very much.

Wilson Baraza Obore: Kwa majina naitwa Wilson Baraza Obore mimi nimzaliwa Bohaya hapa, kwa hivyo ile mimi nataka kuchangia kubwa sana ni kuhusu shamba ya marehemu, mzee anaweza kumuacha nyinyi vijana watatu ama wanne lakini unakuta watu wengine wanaigiza mambo menging fulani wanaenda kushtaki marehemu na bila hata nyinyi wengine kuenda kwa sababu kuna mama, mzee alikuwa na nyumba zake, mbili ama tatu, sasa mimi nataka Commission waendeleo ni huu mpango kwa sababu wanaweza kuangalia maneno wachukue hawa watoto kwa wakati wanaenda kushtaki mzee waende wote, si mtu mmoja ndiyo maneno yangu.

Com.Nunow: nani mwingine nimemuita? Njoo ujadikishe, njoo ujadikishe, Bernard Ojiambo, Peter Obinda, Arther Opendi Thomas Muhuhu, nani yule yuko, Obinda, jina yako, Peter Obinda anaonekana hayuko, Arther Obebi hayuko Thomas Muhuhu, hayuko na John Odanga, akaribie Peter Wandera, Michael Wesonga, yuko? usipoitika sitaweza kujua. Nani yuko? Peter Michael mzee karibia, Julius Chebuche hayuko, Learnard Wesonga, na George Baraza, mpatie mzee mkarishe hapa mbele kwa hiki kiti cha mbele, cha mbele, ya mbele. Sawa Bernard endelea.

Bernard Ojiambo: Kwa majina naitwa Benard Ojiambo, kutoka Constituency ya Nambale. Yangu ni kama yafuatayo, ningependa sheria ibuniwe hospitali za kiserikali itakayo kabiriana na madaktari. Kwa kuwa wagonjwa wetu wanaumia sana. Kwa kutojali wauguzi. Kwa vile kama hujamlipa pesa anazohitaji,, mgonjwa wako hatashughulikiwa vilivyo.

Interjection Com.Nunow: Ungependa nini kwa afya?

Bernard: Ningependa sheria ibuniwe itakayo kabiliana na madaktari wetu, wa hospitali kwa vile mgonjwa, ukipeleka kule mgonjwa kama hauna pesa za kumhonga huyo daktari mgonjwa wako atazidi kuumia hata atakufa pale. Matibabu yapeanwe sawa kwa kila mmoja.

Com.Nunow: Asante sana

Michael Wesonga: Kwa majina naitwa Michael Wesonga Namukuru, mimi yangu yote imeandikwa kwa memorandum na

nitasema tu neno moja ya assistant chief na chief, hawa watu wamezaliwa hapa, hapa kama Buhayo au Wabuhayo. Na waalimu ndio waweze kuwapatia transfer, kwa sababu hao wamesomea course. Kwa sababu hawo wanasomea course ya assistant chief na chief sio wamesomea course ya chief na assistant chief, hawa watu wazaliwa hapa. Asante.

Com.Nunow: Ipeleke huko, Julius Chepcher njoo, njoo uchukuwe njoo tu kwa microphone. Leonard Wesonga yuko, hayuko, na George Baraza, yuko, Julius tupatie majina na point moja.

Julius Chepcher: Mimi kwa majina naitwa Julius Chepcher, na neno langu moja kusalimu viongozi ambao wakuja kututembelea leo, na ni upendo kwangu kujua kwamba neno ambalo tulikuwa nayo yalikuwa mengi lakini kitu ambacho nauliza serikali yetu, irudishe mtido ule ule ulikuwa wa kwanza wa British, masomo iwe ya CPE. Masomo, elimu irudi kwa ile standard ambayo ilikuwapo ya ile ya CPE. Halafu tuanze tena upya form one-form four, and then form four to University. Nafikiria pale tutakuwa na mwendo mzuri sababu wakati tulikuwa na Kenya Equipment Scheme ambayo ilikuwa inatusaidia sisi. Lakini naona wakati huu wazazi kama sisi tuna hangaika sana kwa upande wa elimu ambayo imekunja kama 8-4-4. Sasa hata hayo ambayo ilikuwa ya kwanza ile, inaonekana sasa ile elimu ambayo ilikuwa ya kwanza imekuwa ni kama kati, kati ya secondary school kwa shule ya Primary school. Hapo naomba serikali irudishe mtindo wenye ulikuwa wa kwanza ule ambao tulikuwa tunalipa shilling ishirini kwa term. Halafu tuwe na equipment scheme irudi. Chokaa, serikali ilete, kalamu tulikuwa tunapatiwa kwa shule, kitabu na hali kadhalika. Hapo naona hapo itakuwa mtatusaidia sisi wananchi wengine. Kwa sababu kuna wananchi wengine ambao hawana kazi, na kazi yao wananchi ndio wasomeshe watoto wao, mpaka wapike pombe ya chang'aa ndio wapate malipo yale ambayo yanalipwa kwa shule. Nayo serikali nayo, inafuatilia hao, sasa ikiwakuta kama wametengeneza hiyo ndio wauzie wateja wao, ndio wapate shule wanawashika, na tena kuwanyang'anya yote kabisa ambapo inabaki bure, mtoto anabaki nyumbani huyo mzazi anabaki hivyo, hapo tulikuwa tunaomba tu ni hayo tu. Asante.

Com.Nunow: Inaonekana hatuwezi kuwasikia kwa sababu ya mvua, sasa wale ambao walitaka kuzungumza, ambao wanajua kuandika mtapatiwa ma karatasi muandike points yile mulikuwa mnataka kuzungumzia ili hizo points tupokee na tuweze kwenda naye, kwa sababu itakuwa ni kelele bure hata tape haitaweza kusikika, sawa, sawa, kama ulikuwa unataka kuzungumza njoo hapa mbele upatiwe karatasi uandike points zako. Ziwezi kukusikia hiyo ndio shida hata kwa microphone. Grace give them papers those who want to write, those who do not want to write - Sasa nitapatia Co-ordinator aseme neno moja mbili kisha amualike Chairman wa 3Cs atuongoze kwa kufunya kikao, atupatie mtu wa kutuombea, baada ya yeye kusema machache.

Timothy Wesonga: Asante sana bwana Commissioner, nadhani sasa nafikiria tumefika mwisho wa kikao na bila kupoteza wakati nitamuita Chairman wa 3C's aweze kupeana vote of thanks bwana chairman karibu.

Chairman 3Cs: Commissioners, na wananchi wenzangu, nafikiri namna mmesikia sasa tumefika kikomo na ninafikiri ni kikomo kizuri kawaida ya muafrika kama unamaliza kazi yako halafu mvua inyeshe, mambo huendea vizuri. Kwa hivyo kwa hayo machache nitauliza Zainabu Muyoti a give vote of thanks to wageni wetu, na nyinyi halafu ndio nitamuomba bwana Naftali

